

Kusherehekea Valentine's Day

Qur'an wa Sunnah Society of East Africa (QSSEA) <http://www.qssea.net>



Jee inaruhusiwa kusherehekea Valentine's Day au Sherehe Zengine za Kikafiri?

Kusherehekea Valentine's Day hairuhusiwi kwa sababu nyingi:

1 – Ni sherehe za kubuniwa zisizo na asili yeyote katika sharia.

2 – Inawalingania watu kuhusisha nyoyo na akili zao katika mambo ya kipumbavu yanayo enda kinyume na uongozi wa Salaf – as-Saalih (viongozi wema waliotangulia). Kwa hivyo ni haraam siku hii kufanya mambo yote yanayo husiana na sherehe ya siku hii, kila kinacho husiana na siku hii kama vile vyakula, vinywaji, mavazi, kupeana zawadi na kadhalika. Muislamu anatakiwa akijivunia na dini yake na wala asiwe dhaifu kwa kutaka kufuata kila mwenye kupiga ukelele usio na maana. Namwomba Allah awahifadhi Waislamu kutokama na majaribio haya, yalio wazi na yalio fichika, na kutu simamia sote na kutupa nguvi. Walaahu 'Aalam.

Sheikh Muhammad ibn Saleh al-'Uthaimeen

Ni Haraam kwa Waislamu kusaidia katika sherehe hizi (za Valentine) au sherehe yeyote nyengine ya kiharamu kwa njia yeyote, kama chakula, vinywaji, kununua, kuuza, kutengeneza, kuwasiliana, kutangaza kwa njia yeyote, kwa sababu yote haya yanahisabika kama umechangiwa katika kusambaza na kusaidia katika kufanya madhambi, kupita mipaka, na kumuasi Allah na mtume wake. Allah (Subhanahu Wataala) amesema:

وَتَعَاوَنُوا عَلَىٰ الْبُرْءِ الْقَتْلَىٰ وَلَا تَعَاوَنُوا عَلَىٰ الْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ وَقَاتِلُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ لِيُذْهِبَ اللَّهُ الْأَعْقَابِ

Saidianeni katika al-Birr (kutenda mema) na at-Taqwa; wala msisaidianeni katika dhambi na kupita mipaka. Na mcheni Allah, kwa hakika Allah ni mkali wa kuadhibu. [Sutatul Maidah 5:2]

Basi Waislamu lazima washikamane na Qur'aan na Sunnah katika mambo yao yote, haswa wakati wa fitnah na wakati wa majaribio mengi (kama tulio nao). Lazima awe ni mwenye akili na atahadhari na kujiepusha katika kuzama katika upotofu wa wale walio pata hasira na ghadhabu za Allah na wale walio potea (mayahudi na manasara) na wanao asi ambao hawatarajii chochote kutoka kwa Allah na wala hawaoneshi heshima yeyote kwa dini ya Kiislamu. Muislamu anatakiwa ajilinde kwa Allah na ataka Uongofu kutoka Kwake na amwombe msaada wa kumfanya asitawi katika dini, kwa sababu hakuna anaye ongoza isipokuwa Allah na hakuna atakaye tuwezesha tusimame wima isipokuwa Yeye tu. Na Allah ndiye mwenye Nguvu zote. Tunamwomba Allah amteremshie rehema na amani Mtume Muhammad na familia yake na masahaba wake wote (ameen).

Al-Lajnah al-Daa'imah li'l-Buhooth al-'Ilmiyah wa'l-Iftaa' (Chama cha maUlamaa Saudia)